**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC)

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2023 HADI JANUARI 2024

[Imetolewa chini ya Kifungu cha 136(15) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]

Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole,
S.L.P. 941,
41105 **DODOMA.**

Februari 2024

## IKISIRI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) inawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 (Kanuni za Bunge. Madhumuni ya Taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kubaini hali ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024.

Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi kwa kueleza mambo ya jumla (madhumuni na mawanda), muundo wa taarifa msingi wa shughuli za Kamati na njia zilizotumika kutekeleza shughuli hizo. Sehemu hii inafungua maudhui ya taarifa kwa kurejea Kanuni na miongozo mingine inayohusu shughuli za Kamati na masuala ya uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelezwa ambazo ni uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, ziara za ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na mafunzo ya kujenga uelewa wa pamoja miongoni mwa wajumbe, sehemu hii pia inabainisha matokeo ya uchambuzi ambayo ni kubainika kwa mambo yafuatayo:-

(i) Taasisi za uwekezaji wa Mitaji ya Umma kutopatiwa marejesho ya VAT hata baada ya taratibu zote kukamilika. Kwa mfano STAMIGOLD, GASCO na ETDCO zimechelewesheWa marejesho ya VAT, na hivyo kuathirika kwa ukwasi wa kampuni na mtaji wa umma uliotumia kwa uwekezaji;

(ii) Zipo taasisi za uwekezaji wa Mitaji ya Umma ambazo hazizingatii vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina, vilivyowekwa na Msajili wa Hazina kwa kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na majukumu), Sura ya 370;

(iii) Baadhi ya Taasisi za uwekezaji wa Mitaji ya Umma zinajiendesha bila kuwa na Mpango wa Uwekezaji (*Investment Plan*), hali hii inasababisha taasisi hizo kutokuwa na mwelekeo madhubuti wa kiuwekezaji na kukosa mikakati madhubuti ya kufanikisha uwekezaji;

(iv) Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa uanzishaji na usimamizi wa Kampuni tanzu za taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kunaathiri Ufanisi na tija ya baadhi ya kampuni tanzu;

(v) Benki ya maendeleo inashindwa kujiendesha na kukidhi masharti ya Benki kuu ya Tanzania kutokana na kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 24 tu ili hali kiwango cha chini cha kuruhusiwa kuendelea ni shilingi Bilioni 200. Aidha, Benki hii imeshindwa kulipa amana ya shilingi Bilioni 206.8 zilizowekwa na watu na taasisi za Serikali. Vilevile, Benki imepata hasara ya shilingi bilioni 129 kati ya mwaka 2021 na 2022 kutokana na mikopo chechefu ulifikia asilimia 20%;

(vi) Ufanisi mdogo wa Bodi ya utalii unaochangiwa na uamuzi wa Serikali kuondoa mapato ya Bodi hiyo kupitia Ushuru wa utalii. Aidha, hali hiyo pia imechangiwa na kuwepo kwa taasisi nyingine za utalii zinazotangaza masuala ya Utalii;

(vii) Kuathirika kwa Mitaji ya taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kutokana na kuzidai taasisi nyingine za Serikali. Kwa mfano ETDCO inadai TANESCO na REA sh. Bilioni 44.782 na LATRA inadai TRC na UDART jumla ya shilingi Bilion 3.7;

(viii) Zipo taasisi za uwekezaji wa Mitaji ya Umma zenye changamoto ya kutoa rejesho la uwekezaji (*Returns on investment*) kutokana na usimamizi usio madhubuti wa Serikali pamoja na kutokuwajibika ipasavyo kwa bodi na Menejimenti za taasisi zinazohusika;

(ix) Mtaji wa Mamlaka za Maji unaathirika kutokana na mamlaka hizo kutozwa gharama ya umeme kwa viwango vya kibiashara ili hali mamlaka hizo zinatoa huduma;

(x) Mamlaka za maji zinabebeshwa mzigo wa kugharimia miradi ya majitaka ambayo inagharama kubwa kuliko huduma za majisafi ambazo ni chanzo kikuu cha mapato ya mamlaka hizo. Hali hiyo inaendelea kupunguza mtaji wa mamlaka hizo na hivyo kuathiri utendaji wake na tija iliyokusudiwa; na

(xi) Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) inakabiliwa na changamoto za kiuendeshaji ikiwemo: kukosa taarifa sahihi kuhusu idadi na ukubwa wa Ranchi inazomiliki, kupata hasara na kupungua kwa ufanisi wake. Mambo hayo yana kwamisha NARCO kumudu azma ya kuanzishwa kwake.

Kwa ujumla, sehemu hii ya pili imesisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za kutatua changamoto hizo na kuweka mazingira yenye ufanisi zaidi kwa mitaji ya umma.

Sehemu ya tatu na mwisho inabainisha mapendekezo muhimu kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hizo. Jumla ya mambo kumi na moja yanatolewa mapendekezo ambayo yakipitishwa na Bunge, yanatazamiwa kuwezesha hatua stahiki dhidi ya changamoto hizo.

Mwisho, sehemu hii inamalizia kwa kutoa shukurani na pongezi na mwisho kabisa ni kuhusu hoja kwamba, "Bunge liipokee Taarifa ya Kamati na likubali maoni na mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo".

# YALIYOMO

IKISIRI ..... i

YALIYOMO ..... iv

SEHEMU YA KWANZA ..... 1

1.0 UTANGULIZI ..... 1

1.1 Maelezo ya Awali ..... 1
1.1.1 Madhumuni ..... 1
1.1.2 Mawanda (Scope) ..... 2
1.2 Muundo wa Taarifa ..... 3
1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati ..... 3
1.4 Njia zilizotumika (Methodology) ..... 4

SEHEMU YA PILI ..... 6

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI ..... 6

2.1 Maelezo ya Awali ..... 6
2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ..... 7
2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma Zinazotumia Mitaji ya Umma ..... 7
2.3.1 Rejesho la uwekezaji (return on investment) kwa Serikali ..... 7
2.3.2 Kuchelewesha marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ..... 8
2.3.3 Baadhi ya Mashirika kushindwa kufikia vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ..... 9
2.3.4 Baadhi ya mashirika kutekeleza shughuli za uwekezaji bila kuwa na Mpango wa Uwekezaji (*Investment Plan*) ..... 13
2.3.5 Usimamizi wa Kampuni Tanzu za Mashirika ya Umma ..... 14
2.3.6 Utendaji wa Benki ya Maendeleo ..... 17
2.3.7 Utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ..... 19
2.3.8 Baadhi ya mashirika ya umma kudaiwa na taasisi nyingine za serikali ..... 20
2.3.9 Utendaji wa mamlaka za maji ..... 21
2.3.10 Utendaji wa Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) ..... 24
2.4 Uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji iliyotembelewa na Kamati ..... 26
2.5 Ushiriki katika Semina na warsha Mbalimbali ..... 33

SEHEMU TATU ..... 34

3.0 MAONI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ..... 34

3.1 Maelezo ya Jumla ..... 34
3.1.1 STAMIGOLD na ETDCO kuchelewa kupewa marejesho ya VAT, jumla ya sh. Bilioni 15.9 ambazo ni marejesho ya VAT kwa STAMIGOLD, GASCO na ETDCO ni kiasi ambacho kinaathiri ufanisi katika uwekezaji kutokana na kupungua kwa mtaji. ..... 34
3.1.2 Baadhi ya taasisi na Mashirika ya Umma kushindwa kuzingatia vigezo vya utendaji, licha ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370 kumpa Msajili wa Hazina uwezo wa kupanga vigezo vya utendaji; ..... 34
3.1.3 Taasisi za uwekezaji kujiendesha bila kuwa na mpango wa uwekezaji, jambo linaloathiri Mitaji ya Umma iliyowekezwa kwa taasisi hizo; ..... 34

3.1.4 Uanzishwaji wa Kampuni Tanzu za Taasisi za uwekezaji wa mitaji ya Umma, ambapo imabainika badhi ya kampuni tanzu zinazozorotesha ufanisi wa mitaji ya umma ni jambo linalokinzana na madhumuni ya kuanzishwa kwake; ..... 34
3.1.5 Kushindwa kwa Benki ya Maendeleo kujiendesha ambapo imebainika kuwa Benki hii inakabiliwa na changamoto ya kuwa na mtaji mdogo, kushindwa kukidhi masharti ya Benki ya Tanzania kuhusu kiwango cha mtaji na kushindwa kulipa amana zilizowekwa na watu na taasisi za Serikali; ..... 34
3.1.6 Bodi ya Utalii Tanzania inakabiliwa na changamoto ya sheria iliyoianzisha kuwa imepitwa na wakati na Bodi inauwezo mdogo wa kifedha unaochangiwa na kuondolewa kwa ushuru wa utalii na taasisi nyingine kuendelea kujitangaza;..... 35
3.1.7 Baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuathiriwa na Madeni; .... 35
3.1.8 Changamoto ya Upatikanaji wa Rejesho la Uwekezaji; ..... 35
3.1.9 Utendaji wa Mamlaka za Maji ambapo Mamlaka za Maji zinajumuishwa kwenye malipo ya gharama za umeme kibiashara jambo linalosababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji..... 35
3.2 Mapendekezo ..... 35
3.2.1 Taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma kucheleweshewa marejesho ya VAT..... 35
3.2.2 Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kushindwa kuzingatia vigezo vya utendaji ..... 36
3.2.3 Baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Umma kufanya Shughuli za Uwekezaji bila kuwa na Mpango wa Uwekezaji (Investment Plan) ..... 37
3.2.4 Uanzishwaji wa Kampuni tanzu za Taasisi za Uwekezaji wa Umma usiosimamiwa vema ..... 37
3.2.5 Kushindwa kwa Benki ya Maendeleo kujiendesha ..... 38
3.2.6 Changamoto ya Bodi ya Utalii Tanzania kutokana na Sheria iliyoianzisha ..... 39
3.2.7 Baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuathiriwa na madeni zinazodai taasisi za Serikali. ..... 40
3.2.8 Changamoto ya upatikanaji wa Rejesho la Uwekezaji (Returns on Investment)41
3.2.9 Mamlaka za Maji kutozwa gharama za Huduma ya Umeme kibiashara ..... 42
3.2.10 Mamlaka za Maji kuongezewa mzigo wa kugharamia miradi ya maji taka..... 42
3.2.11 Changamoto ya uendeshaji wa NARCO ..... 43
4.0 HITIMISHO .....45
4.1 Shukurani..... 45
4.2 Hoja..... 47
VIAMBATISHO.....48

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023 ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni hiyo inailazimisha Kamati kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya Shughuli zake, kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Mkutano huu wa Bunge ulioanza tarehe 30 Januari, 2024 ndio Mkutano wa mwisho wa Bunge kabla ya Mkutano wa Bajeti. Bila shaka Maazimio yatakayopitishwa na Bunge kutokana na Taarifa hii yataweza kuzingatiwa katika mchakato wa Bajeti 2024/2025 kama ilivyokusudiwa katika Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge. Hivyo, mjadala wa Bunge kwa mambo yanayobainishwa katika Taarifa hii una umuhimu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufuatilia vizuri mtiririko wa Taarifa hii naomba kueleza kwa ujumla kuhusu madhumuni na mawanda yake kama ifuatavyo:-

#### 1.1.1 Madhumuni

**Mheshimiwa Spika**, kwa ajili ya kurahisisha mjadala na kuliwezesha Bunge kujielekeza kwenye shabaha ya Taarifa hii, napenda kubainisha madhumuni ya Taarifa hii inakusudia kuripoti hali ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliyobainika kutokana na Shughuli za Kamati kwa kipindi kilichoishia Februari, 2024. Shughuli hizo ni zile ambazo hazikuwemo

kwenye Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni tarehe 2 Novemba, 2023 wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge. Lengo ni kuliwezesha Bunge kuwa na picha kamili ya mitaji ya umma kwa wakati muafaka.

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni hayo yanatimizwa kutokana na ufafanuzi wa jumla kuhusu Mitaji ya Umma inayosimamiwa na Serikali au matumizi ya mitaji ya Umma yanavyonufaisha Serikali na Taifa kwa ujumla. Ufafanuzi huo unaliwezesha Bunge kutekeleza Madaraka yake ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

### 1.1.2 Mawanda (Scope)

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufanikisha utambuzi wa mambo yanayostahili kutarajiwa, vigezo, mwelekeo wa maoni na mapendekezo katika hoja ya Kamati, sehemu hii inabainisha mawanda *(scope)* ya Taarifa. Kulingana na madhumuni niliyoyaeleza, Taarifa hii inagusa masuala yafuatayo:-

(i) Hali ya Mitaji ya Umma na Uwekezaji katika Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali au Taasisi nyingine za Umma; na

(ii) Hali ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika vitega uchumi (*investments*) ambapo Serikali ina hisa chache.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli zote za Serikali zinazohusiana na mambo hayo zinafanya uwekezaji wa mitaji ya umma. Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu Shughuli za umma zinazosimamiwa na Serikali kwa kutumia mtaji wa umma unaojumuisha mambo hayo saba.

## 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Kama nilivyotangulia kusema Taarifa hii inawasilishwa kukidhi masharti ya Kanuni za Bunge. Masharti hayo ni Pamoja na muundo wa Taarifa. Miongoni mwa masharti hayo ni kuhusu muundo wa Taarifa ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge inataka Taarifa iwe na sehemu tatu. Taarifa hii inazingatia sharti hilo kwa kugawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla, madhumuni ya taarifa, msingi wa Shughuli za Kamati na njia zilizotumika;

(ii) Sehemu ya pili ambayo inaeleza Shughuli za Kamati na mambo yaliyobainika. Aidha, sehemu hii inafafanua matokeo ya uchambuzi wa taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma; na

(iii) Sehemu ya tatu inayobainisha maoni ya jumla na mapendekezo ya kutatua changamoto zilizobainika. Sehemu hii pia imehitimisha na kutoa hoja.

## 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa shughuli zote za Kamati hii ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Aidha, Ibara ya 63 (2) ya Katiba imelipa Bunge jukumu la kusimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. Vilevile, Kamati imezingatia Kanuni za Kudumu za Bunge na Sheria ya Msajili wa Hazina (mamlaka na majukumu), Sura ya 370.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 11(1) na (2) cha Nyomgeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimebainisha majukumu ya Kamati ambayo ni:-

(i) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

(ii) Kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa kazi za Kamati unatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa shughuli hizo, Kamati imezingatia:-

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011;

(iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001;

(iv) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 370;

(v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992; na

(vi) Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na miongozo hiyo, Kamati ilipokea taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kila shirika na taasisi kadiri zilivyopangwa kulingana na matokeo ya mapitio ya taarifa kuu za msajili wa hazina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, uchambuzi wa taarifa hizo umeiwezesha kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma kama inavyoripotiwa.

## 1.4 Njia zilizotumika (Methodology)

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kufanikisha majukumu ya kamati kama inavyoelekeza Kanuni ya 142

ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti (*reliability*) na ustahiki (*validity*) wa matokeo ya uchambuzi wa Kamati. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge katika kutekeleza majukumu yake, kamati ilitumia njia mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea, kuchambua na kujadili taarifa ya msajili wa hazina kuhusu uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma. Katika kutekeleza hili, kamati ilikutana na taasisi na mashirika ya umma yapatayo hamsini na saba (57). Orodha ya taasisi na mashirika hayo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.01** cha taarifa hii.

(ii) Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya uwekezaji iliyotekelezwa na taasisi na mashirika ya umma. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2023, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na taasisi na mashirika ya umma katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Kagera, Kigoma, Mwanza, Katavi, Geita (Chato) na Singida. Mantiki ya ukaguzi huo ni kuiwezesha kamati kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi husika pamoja na kubaini tija ya uwekezaji unaotekelezwa na taasisi hizo. Miradi iliyotembelewa inaonekana katika **Kiambatisho Na. 02** cha Taarifa hii; na

(iii) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na taasisi na mashirika ya umma na wadau mbalimbali.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa madhumuni ya utaratibu wa kuripoti shughuli za Kamati ni kuliwezesha Bunge kubaini mambo ya kupatiwa ufumbuzi, napenda kubainisha Shughuli zilizotekelezwa. Aidha, nabainisha mambo yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo ili kuliwezesha Bunge kuyajadili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia dhima na majukumu ya Kamati hii, Shughuli zinazoripotiwa pamoja na yaliyojitokeza zinahusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Uchambuzi wa taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma kwa lengo la kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kwamba, umezingatia taratibu, sheria na miongozo mingine mujarabu ya biashara kama inavyoelekezwa na kifungu cha 11(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

(ii) Ziara za ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji wa umma kwa lengo la kubaini iwapo utekelezaji wake unazingatia miongozo ya uwekezaji wa umma; na

(iii) Kupata mafunzo mbalimbali yanayohusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yaliyotolewa na taasisi na mashirika mbalimbali ya umma. Mafunzo hayo yameiwezesha Kamati kutoa ushauri kwa taasisi hizo kwa lengo la kuboresha utendaji wao na kupata tija inayokusudiwa.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma zinazohusu uwekezaji. Lengo la Bunge ni kujiridhisha iwapo uwekezaji uliofanywa na Serikali katika taasisi na mashirika hayo una tija na kama umezingatia sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ya biashara. Katika kufanya hivyo, Kamati ilipitia taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma katika mashirika na taasisi za umma hamsini na saba (57)

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya hoja na masuala yaliyochambuliwa kwa kipindi cha Februari, 2023 hadi Januari, 2024 yamekwisharipotiwa kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mwezi Novemba, 2023, iliyokuwa na jumla ya maazimio kumi na nne (14), Kamati inaendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio hayo.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma Zinazotumia Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua utendaji wa taasisi na mashirika ya umma ili kujiridhisha kama uwekezaji katika mashirika na taasisi hizo ni wa ufanisi na tija ya uwekezaji inapatikana. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha mambo yafuatayo: -

### 2.3.1 Rejesho la uwekezaji (return on investment) kwa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwaka 2021/2022 thamani ya uwekezaji wa mitaji ya umma uliofanywa na Serikali ulikuwa ni jumla ya **Shilingi trilioni 73.36** ambapo **Shilingi trilioni 70.8** ni thamani ya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma ambayo Serikali ina umiliki wa hisa zaidi ya asilimia 51 na **shilingi trilioni 2.56** ni thamani ya uwekezaji wa Serikali katika kampuni 40 ambazo ina umiliki wa hisa chache.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uwekezaji huo Serikali ilipata gawio la jumla ya **shilingi bilioni 850** mchanganuo wa gawio hili unaonesha kuwa, **shilingi bilioni 645** zilitokana na rejesho kutoka kwenye mashirika ya umma na **shilingi bilioni 204** ni gawio kutoka kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganifu wa mtaji wa Serikali na rejesho lake kwenye kampuni ambazo ina hisa chache na mtaji wa Serikali na rejesho lake kutoka kwenye mashirika ambayo ina hisa nyingi, unadhihirisha kuwa Serikali imekuwa ikipokea rejesho kubwa kutoka kule ilikowekeza hisa chache. Ni mtazamo wa kamati kuwa, ipo haja ya Serikali kufanya tathimini juu ya hili na kutafuta namna ya kuongeza mtaji kwenye kampuni ambazo ina hisa chache ili iweze kunufaika zaidi.

### 2.3.2 Kuchelewesha marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

**Mheshimiwa Spika,** sheria ya kodi ya ongezeko la thamani ya Tanzania (VAT Act) imeweka utaratibu unaowawezesha walipa kodi waliosajiliwa kwenye kodi ya VAT kuomba kurejeshewa VAT iliyolipwa kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma ambazo wametumia katika shughuli zao za biashara. Fedha hizi hupaswa kurudishwa kwa wahusika kwa kipindi cha miezi mitatu mpaka kumi na mbili baada ya kuwasiisha nyaraka za kuomba marejesho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na kampuni tanzu mbalimbali kwa ajili ya kuangalia namna zinavyotekeleza majukumu yake. Moja ya changamoto ambayo Kamati iliibaini

ni ucheleweshwaji wa marejesho ya VAT, jambo linaloathiri mitaji ya kampuni hizo na kuzipunguzia ufanisi. Miongoni mwa kampuni ambazo zimekumbana na ucheleweshaji wa marejesho hayo ni STAMIGOLD inayodai **shilingi Bilioni 12.3**, GASCO inayodai **shilingi bilioni 3.01** na ETDCO inayodai **shilingi milioni 563**.

**Mheshimiwa Spika,** ucheleweshaji wa marejesho ya VAT unapunguza mapato, unaathiri utendaji wa kampuni hizo na kupunguza ufanisi wa ujumla. Mfano kwa STAMIGOLD deni la VAT limeongezeka kutoka **shilingi bilioni 4.1** mwaka 2019/2020 na kufikia **shilingi bilioni 12.3** mwaka 2021/22. Ulinganisho wa deni la Kodi ya VAT na mapato ya Kampuni ni sawa na asilimia 9.2 na asilimia 30.2 mtawalia. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa STAMIGOLD inajiendesha ikiwa na mtaji hasi kwa kiasi cha **shilingi bilioni 11.7**, kwa maana kuwa, endapo wakirejeshewa fedha wanayodai ambalo ni **Shilingi Bilioni 12.3**, Kampuni itaweza kurudi kuwa na mtaji chanya. Ni maoni ya Kamati kuwa, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itekeleze sharti la kisheria la kurejesha fedha hizi kwa wahusika kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

### 2.3.3 Baadhi ya Mashirika kushindwa kufikia vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 (Madaraka na Majukumu), Msajli wa Hazina ana jukumu la kuzipangia taasisi na mashirika ya umma vigezo vya utendaji kwa lengo la kuziongoza kujiendesha kwa ufanisi na kupata tija ya uwekezaji. Katika uchambuzi wa taarifa za utendaji wa taasisi na mashirika mbalimbali, kamati imepitia

vigezo hivyo na kubaini kuwa baadhi ya mashirika yamekuwa yakijiendesha nje ya vigezo hivyo kama ifuatavyo: -

**(a) Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini**

**Mheshimiwa Spika,** kigezo hiki kinayataka mashirika ya umma kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini kila mwaka. Ili kuweza kutekeleza hili, taasisi na mashirika ya umma yanapaswa kuongeza mapato yake kwa kuongeza ufanisi katika makusanyo, kuzalisha vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha mikakati ya ukusanyaji wa mapato, kwani kasi ya ukuaji wa mapato ndiyo itachangia kupungua kwa utegemezi wa ruzuku. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, baadhi ya taasisi na mashirika bado yanategemea ruzuku ya serikali kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na mapato ya ndani. Baadhi ya Mashirika hayo ni pamoja na Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Shirika la viwango Tanzania (TBS), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Benki ya Maendeleo TIB (DFI) na Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Uchambuzi unaonesha kwamba, Utegemezi huu unaongeza mzigo kwa Serikali, hivyo basi kwa kuzingatia fursa zilizopo, mashirika haya yasimamiwe kikamilifu ili yaweze kuongeza ufanisi wake ili ziweze kupunguza au kuondokana kabisa na utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

**(b) Ukuaji wa Mapato**

**Mheshimiwa Spika,** kigezo hiki kinaelekeza taasisi na mashirika ya umma kukuza mapato yake kwa kiwango kisichopungua asilimia 10 kila mwaka, ili kukabiliana na ongezeko la matumizi ambalo linaweza kusababishwa na mfumuko wa bei.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mashirika yafuatayo hayana mwenendo himilivu wa ukuaji wa mapato:- Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Shirika la Masoko Kariakoo(KMC). Jambo hili linaloathiri uwezo wa mashirika kujiendesha kwa ufanisi, hivyo basi Kamati inaona kuna haja ya Serikali kuongeza usimamizi kwa taasisi na mashirika ya umma ili ziweze kujiendesha kwa ufanisi na kuweza kuongeza mapato.

**(c) Uwiano wa madeni ya muda mfupi kwa mali za muda mfupi**

**Mheshimiwa Spika**, kigezo hiki kinapima hali ya ukwasi wa taasisi au shirika la umma, ambapo kinataka uwiano wa 2:1 hii ikiwa na maana kwamba, mali za muda mfupi zinapaswa kuwa mara mbili ya madeni ya muda mfupi. Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa, baadhi ya mashirika yaliyofika mbele ya Kamati hayana uwezo wa kumudu kulipa madeni ya muda mfupi kwa kutumia mali za muda mfupi. Mashirika hayo ni pamoja na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Mfuko wa Taifa wa Pembejeo (AGITF), Bohari ya Dawa (MSD). Uwiano usio mzuri wa madeni ya muda mfupi na mali za muda mfupi unaathiri uwezo wa shirika kuweza kulipa madeni yake pindi yanapojitokeza, ni vema Serikali ikaongeza usimamizi ili mashirika haya yaweze kuongeza ukwasi wake.

**(d) Rejesho la mtaji**

**Mheshimiwa Spika,** kigezo hiki kinapima ufanisi wa mtaji uliowekezwa katika mashirika ya umma, ambapo kigezo kilichowekwa na Msajili wa Hazina ni asilimia 15. Kupitia kigezo hiki inawezekana kutambua maeneo yanayofanya vizuri na ambayo hayafanyi vizuri. Kupitia rejesho la mtaji, Serikali inaweza kutambua maeneo ambayo uwekezaji unaweza kuongezeka au kupungua. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mashirika ambayo hayajafikia kigezo hiki ni pamoja na Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC). Kutofikiwa kwa kigezo hiki kumetokana na mashirika hayo kupata faida chini ya asilimia 15 katika miaka mitatu iliyofanyiwa uchambuzi, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iongeze usimamizi ili mashirika haya yaweze kuongeza ufanisi, faida na tija ya uwekezaji iweze kupatikana.

**(e) Ukomo wa gharama za uendeshaji (opex limit)**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa sheria ya Msajili wa Hazina sura 370, ukomo wa gharama za matumizi ukitoa mishahara unatakiwa usizidi asilimia 60. Lengo la ukomo wa matumizi ni kudhibiti gharama za uendeshaji na kuongeza faida au ziada kwa taasisi na mashirika ya umma. Ongezeko la ziada litaongeza mchango wa mashirika hayo kwenda mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa hesabu za baadhi ya mashirika ya umma, umebainisha kuwa, baadhi ya mashirika

ya umma yamekuwa yakikiuka kigezo hiki na kusababisha mchango wa mashirika hayo kwa Serikali kupungua. Baadhi ya mashirika yaliyokutwa na kasoro hii ni pamoja na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), ni maoni ya Kamati kuwa, mashirika haya yasimamiwe kikamilifu ili kuhakikisha yanazingatia kigezo hiki.

### 2.3.4 Baadhi ya mashirika kutekeleza shughuli za uwekezaji bila kuwa na Mpango wa Uwekezaji (*Investment Plan*)

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Uwekezaji (*Investment Plan*) kwa mashirika yenye uwekezaji ni moja ya nyenzo muhimu inayotoa muongozo wa shirika kujua maeneo ya kuelekeza mtaji na picha ya rejesho linaloweza kupatikana. Aidha, mpango wa uwekezaji (investment plan) ni nyenzo ya kujitathimini kwa uwekezaji uliofanyika. Pamoja na umuhimu wa nyenzo hii, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya mashirika yanajiendesha bila kuwa na mpango wa uwekezaji ikiwemo Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) na Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC). Jambo hili limesababisha mashirika husika kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja hivyo kukumbana na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali na kusababisha miradi hii kutekelezwa kwa muda mrefu na hivyo kukosekana kwa tija katika mitaji iliyowekezwa na Serikali kupitia mashirika husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri serikali kuyasimamia mashirika yote yanayotekeleza shughuli za uwekezaji kuhakikisha yanaandaa mpango wa uwekezaji na kuutekeleza kikamilifu.

### 2.3.5 Usimamizi wa Kampuni Tanzu za Mashirika ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** kampuni tanzu ni kampuni zinazoanzishwa na shirika mama ambalo lina umiliki wa hisa zaidi ya asilimia 50 kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake mahususi ikiwemo kuboresha huduma na kuongeza ufanisi. Aidha, taasisi na mashirika ya umma huanzisha Kampuni Tanzu ili zijiendeshe kibiashara na kupata fedha za kuyasaidia kwa njia ya gawio na faida kutokana na uwekezaji uliofanyika katika kampuni tanzu.

**Mheshimiwa Spika**, Msajili wa Hazina ametoa muongozo wa uanzishaji wa kampuni tanzu ambapo shirika mama linapaswa kutekeleza mambo kadhaa ikiwemo kufanya upembuzi yakinifu, kuandaa mpango wa biashara (business plan), katiba na sheria ya kampuni tanzu na kupata ridhaa ya Wizara mama. Mengine ni kupata idhini ya bodi ya wakurugenzi wa shirika mama, idhini ya Msajili wa Hazina na kuandaa bajeti na mpango mkakati wa kampuni tanzu.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa na muongozo huo ulioandaliwa na Msajili wa Hazina ambae ni msimamizi mkuu wa mashirika ya umma yanayoanzisha kampuni tanzu, uchambuzi wa Kamati kuhusu kampuni tanzu zilizofika mbele ya Kamati ulibaini changamoto mbalimbali zikiwemo:-

(i) Kampuni tanzu hazipewi mtaji wa kujiendesha, hivyo zimekuwa zikitekeleza majukumu yake kama idara za

mashirika mama, kwani shirika au kampuni mama inapokuwa na shughuli ya kufanya inayoendana na kampuni tanzu, ndipo hutenga bajeti na kuipatia kampuni tanzu ili itekeleze.

Mfano; kampuni ya kutengeneza nguzo za zege Tanzania (TCPM) ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO iliyopewa jukumu la msingi la kuanzisha viwanda vya nguzo za zege na kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini. Hata hivyo, ni takribani miaka kumi sasa tangu ilipoanzishwa Disemba, 2014 lakini haijaanza kutekeleza jukumu hilo kwani hawajapatiwa mtaji/bajeti. Hii ni kinyume na muongozo wa Msajili wa Hazina ambao unaelekeza kwamba, wakati wa uanzishaji wa kampuni tanzu bajeti inatakiwa kuwa imetengwa.

Kwa sasa TANESCO inaitumia kampuni tanzu hii kama wakala wa kununua nguzo za aina hiyo kutoka kampuni nyingine, jambo ambalo halikuwa jukumu la msingi la kuanzishwa kwake.

(ii) Hakuna mpaka halisi (clear line) wa uendeshaji wa kampuni tanzu. Kampuni mama zimekuwa ndio waendeshaji na watoa maamuzi wakuu wa kampuni tanzu, licha ya muongozo kutaka iwepo katiba na sheria ya kampuni tanzu ambayo itaonesha;- muundo na mgawanyo wa majukumu, miundo na maendeleo ya watumishi, kanuni za fedha na kanuni za kiutumishi.

Uchambuzi kuhusu kampuni tanzu zilizofika mbele ya kamati umebaini kuwa shirika au kampuni mama zimekuwa zikifanya maamuzi katika kampuni tanzu, na

hata watumishi wa kampuni tanzu ni wale wale wa shirika au kampuni mama. Mfano ni TANOIL na GASCO ambazo ni kampuni tanzu za TPDC, ambapo mwenyekiti wa bodi wa kampuni tanzu hizi mbili ni mmoja, lakini pia ni mtumishi wa (TPDC) ambalo ni shirika mama.

(iii) Baadhi ya Kampuni tanzu zimekuwa zikitekeleza kazi/miradi ya kampuni mama bila kuwa na mikataba ya utekelezaji (service level agreement). Kamati imebaini changamoto hii kwa kampuni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme (ETDCO) ambayo ni kampuni tanzu ya TANESCO, ambapo baadhi ya shughuli za TANESCO zimekuwa zikipelekwa ETDCO bila kuwa na makubaliano ya utekelezaji (service level agreement).

(iv) Kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa Kampuni Tanzu, baadhi ya kampuni zimekuwa zikianzisha Kampuni Tanzu bila kufuata muongozo uliowekwa na Msajili wa Hazina, jambo linalopelekea hata usimamizi wake kutokuwa mzuri na hivyo kukosekana kwa ufanisi na tija ya uwekezaji.

Uchambuzi wa Kamati umebaini dosari katika usimamizi wa Mtaji wa Umma uliowekezwa kwa Kampuni ya TANOIL ambayo ni kampuni tanzu ya TPDC na imepewa jukumu la uagizaji na usambazaji wa nishati ya mafuta. Dosari zilizobainika ni pamoja na:-

a) Kukua kwa madeni ya muda mfupi ya Kampuni ambapo madeni hayo yaliongezeka kwa asilimia zaidi ya 100 kutoka shilingi bilioni 6.8 mwaka 2020/21. kufikia

shilingi bilioni 30.0 mwaka 2021/2022, ongezeko hili ni la zaidi ya asilimia 100.

b) Kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo kampuni imekuwa ikipata hasara na hasara hii imeongezeka kutoka **Shilingi milioni 166 mwaka 2020/21** hadi kufikia **shilingi bilioni 7.83,** ongezeko hili ni zaidi ya asilimia 4,000, hasara hii kwa kiasi kikubwa imesababishwa na kuuza mafuta kwa bei ya chini ya bei iliyopangwa na EWURA.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa mambo hayo, Kamati inaona ni muhimu sasa uwekwe utaratibu mahususi ambapo Serikali itahakikisha Msajili wa Hazina anashirikishwa katika hatua zote za uanzishaji, uwekaji wa mtaji na uendeshaji wa biashara zinazofanywa na kampuni tanzu. Utaratibu huu uhusishe kuweka takwa la kisheria la kuyaelekeza mashirika ya umma kumpatia Msajili wa Hazina walau hisa chache kwa lengo la kumuwezesha kuingia katika mchakato wote wa uanzishaji na uendeshaji wa kampuni hizi kwa lengo la kuleta ufanisi pamoja na uwajibikaji (*accountability*).

### 2.3.6 Utendaji wa Benki ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, benki ya maendeleo - TIB imepewa jukumu la msingi la kutoa huduma za kifedha kwenye miradi ya maendeleo kwa gharama nafuu ili kujenga taifa lenye uchumi shirikishi, mseto, mahiri na wenye ushindani. Kwa muktadha huu, benki hii inapaswa kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu na wa kati kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa sasa benki hii haina vigezo vya kujiendesha kama benki kwa mujibu wa vigezo vilivyotolewa na Msajili wa Hazina lakini pia vigezo vya benki kuu ya Tanzania (BOT).

Kwa mujibu wa masharti ya BOT, ili benki iweze kujiendesha inapaswa kuwa na mtaji usiopungua **shilingi bilioni 200.** Benki ya maendeleo TIB (DFI) ina mtaji wa **shilingi bilioni 24,** changamoto hii pia imesababisha benki hii kushindwa kulipa amana (FDR) za jumla ya **shilingi bilioni 206.85** zilizowekwa na watu na baadhi ya taasisi za Serikali. Amana hizi zimefika muda wa kurejeshwa lakini kutokana na hali mbaya ya ukwasi, benki imeshindwa kuzirejesha.

Aidha, benki imepata hasara kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, mwaka 2021 na 2022 na hasara kubwa imepatikana mwaka 2022 ambayo ni **shilingi bilioni 195.91**. Hasara hii ilitokana na kuongezeka kwa tengo la mikopo chechefu, hadi **asilimia 20** sawa na **shilingi bilioni 159.73** wakati ukomo uliowekwa na BOT ni asilimia 5.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla benki ya TIB (DFI) ina hali mbaya, na kwa kuzingatia umuhimu wa uwepo wa benki hii, ni rai ya Kamati kwamba, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kuiwezesha kupata mtaji toshelevu, sambamba na hilo TIB inahitaji mifumo imara ya uendeshaji wa shughuli za benki hususani mfumo wa uchakakataji maombi ya mikopo na ufuatiliaji ili kuiwezesha benki kutozalisha mikopo chechefu mingine.

**Aidha,** TIB bado inaendesha dirisha la kilimo, jukumu ambalo linaendana na jukumu la msingi la benki ya maendeleo ya kilimo (TADB). Ni vema jukumu hili likapelekwa TADB kwa lengo la kuipunguzia TIB mzigo/majukumu, lakini pia TADB italitekeleza jukumu hili kwa ufanisi zaidi.

**Vilevile,** Benki ya Maendeleo TIB(DFI) imekabidhiwa majukumu mengine mengi ambayo kimsingi si sehemu ya jukumu la msingi la benki hii, majukumu hayo ni pamoja na usimamizi wa Mradi wa Kuendeleza na kusambaza Nishati Jadidifu Tanzania TEDAP; Mradi wa Usambazaji wa Majiko yanayotumia Nishati Mbadala kwa ajili ya kupunguza matumizi ya mkaa; Mashamba ya Maua – Arusha; Mradi wa Upanuzi wa Nishati ya Umeme Vijijini – TREEP; Mradi wa Kuchagiza matumizi ya Umeme jua katika kusukuma maji katika Jumuiya za Watumia Maji Vijijini; Kiwanda cha kusindika Nyama (SAAFI; na Benki ya Nyumba (THB). Ni rai ya kamati kuwa majukumu haya yarejeshwe kwa Wizara za kisekta ili kuipunguzia TIB majukumu na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.3.7 Utendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) imepewa majukumu ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, kuhamasisha uendelezaji wa miundombinu ya utalii, kufanya utafiti wa utalii na kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa sekta ya utalii. Kwa msingi wa majukumu haya, bodi inahitaji bajeti ya kutosha ili iweze kuyatekeleza kwa ukamilifu na kwa ufanisi. Hata hivyo, bodi inategemea ruzuku kutoka Serikalini, ambayo imekuwa hailingani na uhalisia wa mahitaji ya bodi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuangalia uzoefu wa nchi nyingine kwenye sekta ya utalii, bodi inapaswa kupewa kipaumbele kwa kutengewa bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleleza majukumu yake kikamilifu kwa lengo la kuvutia na kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini. Tanzania ina vivutio vingi

vikubwa na vya kipekee lakini idadi ya watalii wanaotembelea vivutio hivyo ni wachache na mapato yanayopatikana ni kidogo.

**Mheshimiwa Spika,** bajeti inayotengwa ikilinganishwa na mipango ya bodi ya utalii katika kuimarisha na kuitangaza sekta ya utalii ndani na nje, inaonesha kwamba bodi haitaweza kufikia malengo tarajiwa. Awali bodi ilipewa fursa ya kukusanya kodi ya utalii (*Tourisim Development Levy*) ambayo ilichangia kuongeza mapato na kuiwezesha bodi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kodi hii iliondolewa na kuingizwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali kuanzia mwaka 2020/21, ni ushauri wa kamati kwamba, ili bodi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ni vema kodi hii ikarudishwa kwa bodi.

Aidha, ingawa sheria iliyoianzisha bodi ya utalii, Sura Na. 364 ya mwaka 1962 imefanyiwa marekebisho mara kadhaa, Kamati inaona bado ni ya muda mrefu na haiendani na kasi ya mabadiliko ya dunia katika sekta ya utalii. Ili kuimarisha sekta ya utalii nchini ni vema ikatungwa sheria mpya ambayo itazingatia kasi ya mabadiliko ya dunia, uhitaji wa muundo mpya wa kitaasisi na kuzingatia uzoefu wa nchi zilizofanikiwa katika kuendesha sekta ya utaliii duniani.

### 2.3.8 Baadhi ya mashirika ya umma kudaiwa na taasisi nyingine za serikali

**Mheshimiwa Spika,** kigezo kimojawapo kinachotumika kupima utendaji wa mashirika na taasisi za umma ni uwezo wa kukusanya madeni inayodai (receivables). Kutofanya vizuri kwa kigezo hicho kunaweza kuondoa ufanisi wa kiutendaji.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, baadhi ya mashirika ya umma yanakosa mbinu mbadala na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni (*receivables*) ili kuongeza ukwasi wa shirika na mapato ya Serikali kwa ujumla.

Aidha, kamati imebaini kuwa kwa baadhi ya mashirika ya umma madeni yanatokana na kuzidai taasisi nyingine za Serikali ambazo zinapatiwa huduma lakini hazilipi kwa wakati. Baadhi ya taasisi ambazo Kamati imebaini changamoto hii ni pamoja na kampuni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme (*ETDCO*) ambayo inaidai TANESCO na REA jumla ya **shilingi bilioni 44.78**. Aidha, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA) inalidai Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) jumla ya **shilingi bilioni 1.81** na Kampuni ya *UDART* **Shilingi bilioni 1.9**.

**Mheshimiwa Spika,** madeni haya yanaathiri mizania ya taasisi inayodaiwa lakini pia yanaathiri mizania ya taasisi inayodai na kupunguza ukwasi na ufanisi wa taasisi husika. Ni vema Serikali ikasimamia kiukamilifu taasisi zinazodaiwa ili ziweze kulipa madeni yake kwa wakati.

### 2.3.9 Utendaji wa mamlaka za maji

**Mheshimiwa Spika,** mamlaka za maji nchini ni taasisi za umma zilizoanzishwa kwa minajili ya kutoa huduma (taasisi za huduma) ya majisafi na usafi wa mazingira kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya utoaji wa huduma za majisafi, usafi wa mazingira, usimamizi wa rasilimali za maji na viwango vya ubora wa maji. Katika kutekeleza jukumu hili mamlaka hizi zinakumbana na changamoto mbalimbali zinazosababisha

gharama za uendeshaji kuwa kubwa. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Gharama kubwa za umeme. Uzalishaji wa maji unatumia umeme katika kuendesha mitambo ya uzalishaji wa maji jambo linalosababisha mamlaka hizi kuingia gharama kubwa ya umeme na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa mamlaka. Kamati ilibaini changamoto hii katika mamlaka zifuatazo:-

(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ambayo gharama za umeme zilipanda kutoka shilingi **bilioni 26.64** mwaka 2020/21 hadi shilingi **bilioni 28.89** mwaka 2021/22 ikilinganishwa na jumla ya gharama za matumizi ya Mamlaka ambazo zilikuwa shilingi **bilioni 149.90** na shilingi **bilioni 167.22** kwa mwaka 2020/21 na 2021/22 mtawalia. Ulinganisho wa gharama za umeme kwa jumla ya gharama zote ni sawa na asilimia 17.8 kwa asilimia 17.3 mtawalia;

(ii) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) ilitumia kiasi cha shilingi **Bilioni 5.8** kwa ajili ya gharama za umeme kwa mwaka 2020/21 ambazo ziliongezeka hadi kufikia **bilioni 7.4** mwaka 2021/22 ikilinganishwa na jumla ya matumizi ya mamlaka ambayo yalikuwa shilingi **bilioni 26.5** na shilingi **bilioni 32.3** sawa na uwiano wa asilimia 22 na asilimia 23 kwa mwaka 2020/21 na 2021/22 mtawalia; na

(iii) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGA UWASA) ilitumia kiasi cha shilingi **milioni**

**980** kwa ajili ya gharama za umeme kwa mwaka 2020/21 ambazo ziliongezeka hadi kufikia shilingi **bilioni 1.24** mwaka 2021/22 ikilinganishwa na jumla ya matumizi ya kiasi cha shilingi **bilioni 15.99** na shilingi **bilioni 17.82** sawa na uwiano wa asilimia 6 na asilimia 7 kwa mwaka 2020/21 na 2021/22 mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hizi zimekusudiwa kutoa huduma, kwa muktadha huo ipo haja ya Serikali kutathimini gharama na kuangalia uwezekano wa kuzipatia viwango vya kihuduma ili kuzipunguzia mzigo na kuongeza ufanisi wake.

(b) Uzito wa jukumu la usimamizi wa mazingira pamoja na kodi ya VAT kwenye majitaka. Gharama za uendeshaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira ziko juu hususani kipengele cha majitaka ambapo ujenzi wa miundombinu ya majitaka ni gharama lakini bei inayotozwa kwa watumiaji wa miundombinu hiyo ni ndogo, ambayo pia imekuwa ikitozwa kodi ya VAT.

Kimsingi waratibu wa shughuli ya usimamizi wa mazingira ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira pamoja na NEMC ambao wamekuwa wakipata fedha za miradi ya usimamizi wa mazingira. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali ione haja ya kuzisaidia mamlaka za maji kwa kuzipunguzia jukumu hili au kiasi cha fedha hizo za ufadhili zilekezwe kwenye mamlaka za maji ili kuziwezesha kutekeleza kikamilifu jukumu hili la usimamizi wa mazingira.

(c) Madeni (receivables), Mamlaka za maji zilizofika mbele ya kamati zinakabiliwa na kiasi kikubwa cha madeni ambayo zinadai kwa watumiaji wa huduma ya maji, na kwa kiasi kikubwa madeni haya yanadaiwa kwa taasisi nyingine za Serikali. Madeni haya yanaathiri ukwasi wa mamlaka za maji na ufanisi wa mamlaka kwa ujumla. Kamati imebaini changamoto ya madeni (receivables) kwa mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ambayo inavidai vyombo vya ulinzi na usalama jumla ya **shilingi bilioni 13.9**.

Aidha, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) inazidai Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma (*General Hospital*) na Hospitali ya Milembe pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama vya mkoani Dodoma jumla ya **shilingi bilioni 1.4** kutokana na huduma ya maji waliyopatiwa. Vilevile, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGA UWASA) inadai vyombo vya ulizi na usalama vya mkoani Tanga, Mamlaka ya Bandari (TPA), Hospitali ya mkoa na taaassi nyingine za Serikali jumla ya **shilingi bilioni 1.7.**

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi mamlaka za maji ni taasisi za kihuduma hivyo kuzipatia unafuu katika utekelezaji wa majukumu yake kutaongeza ufanisi na kuleta tija katika kutoa huduma kwa ajili ya ustawi wa jamii.

### 2.3.10 Utendaji wa Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO)

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Ranchi za Taifa (*National Ranching Company Limited-NARCO*) ilianzishwa chini ya Sheria ya Makampuni (Sura 212), ikiwa kampuni tanzu chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (National *Development Corporation*

*NDC),* kwa sasa kampuni hii inajitegemea. Majukumu ya msingi ya NARCO ni kushughulikia ufugaji wa kisasa wa ng'ombe hususani ng'ombe wa nyama kwenye mashamba makubwa ya kibiashara na kuzalisha na kusambaza mbegu bora kwa wafugaji.

Mpango mkakati wa NARCO wa miaka 10 kuanzia mwaka 2019 hadi 2028 ulilenga kuboresha maeneo makuu manne ambayo ni kuboresha ufanyaji wa biashara (core business process), usimamizi wa rasilimali fedha (financial management), kuboresha huduma kwa wateja (excellent customer services) na kuwa na watumishi bora na wenye morali (high quality and motivated employees). Uboreshaji wa maeneo hayo, utasaidia kuongeza mauzo ya kampuni kwa kipindi cha miaka 10 kufikia jumla ya **shilingi bilioni 7.23** kuongeza mtaji wa kampuni kufikia **shilingi bilioni 64.6**.

Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa hakuna fedha zilizowekezwa kwa kampuni ya NARCO kuendana na mpango mkakati wa kampuni wa miaka 10. Sambamba na hilo uchambuzi umebaini kuwa, mapato ya kampuni yamepungua zaidi kutoka **shilingi bilioni 12.26** mwaka 2020/21 hadi **shilingi bilioni 5.86** mwaka 2021/22 sawa na upungufu wa asilimia 52.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine iliyobainika ni kwamba kampuni imekuwa ikipata faida ndogo na kwa mwaka wa fedha 2020/21 ilipata hasara ya **shilingi bilioni 1.17**. Ufanisi hafifu wa kampuni umesababisha athari kwa mtaji wa kampuni ambao kwa miaka miwili mfululizo umepungua kutoka **shilingi bilioni 150.85** mwaka 2020/21 hadi **shilingi bilioni 149.38** mwaka 2021/22.

Aidha, kamati ilibaini kuwa NARCO haina taarifa sahihi ya idadi ya Ranchi inazomiliki pamoja na ukubwa wa rachi hizo, na hilo lilitokana na migogoro mbalimbali inayoendelea katika ranchi za NARCO ikiwemo migogoro katika mkoa wa Kagera.

**Vilevile**, uchambuzi zaidi umebaini kuwa kampuni inatoza ada ya kiasi cha **shilingi Elfu Tatu na Mia Tano (3,500)** kwa ekari kwa mwaka kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na uhalisia. Kiwango hiki cha ada kinasababisha wanaopatiwa maeneo hayo wayakodishe (sub-letting) kwa wafugaji na kujipatia kipato zaidi ambacho kilipaswa kwenda NARCO.

**Mheshimiwa Spika,** ni mtazamo wa Kamati kwamba, ipo haja ya Serikali kufanya tathimini ya kina ya uendeshaji wa NARCO kwa lengo la kuiboresha na kuiongezea ufanisi ili tija ya uwekezaji iweze kupatikana.

## 2.4 Uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji iliyotembelewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Machi, 2023, Kamati ilifanya ziara za kukagua miradi ya uwekezaji ili kujiridhisha kama kuna tija ya kuwekeza mitaji ya umma katika miradi hiyo. Ziara ilifanyika katika mikoa nane (8) ambayo ni Dodoma, Tabora, Katavi, Kigoma, Kagera, Geita, Mwanza na Singida na kuhusisha miradi ishirini na nne (24). Miradi iliyotembelewa imegawanyika katika maeneo manne (4) kama ifuatavyo:-

(i) Miradi ya ujenzi wa miundombinu;

(ii) Miradi ya maji;

(iii) Miradi ya nishati; na

(iv) Miradi ya utalii na huduma.

**(a) Miradi ya ujenzi wa miundombinu**

**(i) Mradi wa ujenzi wa nyumba 1000 Jijini Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha ujenzi wa nyumba 1000 katika jiji la Dodoma, kwa gharama ya shilingi bilioni 20 ambazo ni fedha za mkopo kutoka Serikalini na zinazotumika kama mtaji (revolving fund). Mradi unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza ndio imeanza na inahusisha ujenzi wa nyumba 400; ambapo nyumba 100 na duka moja vimejengwa Chamwino na nyumba 300 zinajengwa Iyumbu.

Mradi huu umelenga kusaidia upatikanaji wa makazi hasa baada ya Serikali kuamua kuhamishia shughuli za Serikali mkoani Dodoma. Hivyo, kukamilika kwake kutapunguza changamoto ya upatikanaji wa makazi na kuwezesha shughuli mbalimbali za kijamii kufanyika katika maeneo ya mradi. Ni ushauri wa Kamati kuwa, shirika lihakikishe mradi huu unakamilika kwa wakati kwa lengo la kupata tija iliyokusudiwa;

**(ii) Mradi wa ujenzi na uendelezaji wa bandari ya Karema**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi na uendelezaji wa bandari ya Karema, na unatekelezwa kwa lengo la kuwezesha wadau katika mnyororo wa biashara kunufaika na fursa za masoko ya bidhaa mbalimbali katika masoko ya nchi jirani. Gharama za mradi ni **shilingi bilioni 47.97** ikijumuisha kodi ya VAT ambazo ni fedha za ndani. Kwa manufaa mapana ya mradi huu katika kuleta tija kwa shughuli za uchumi kwa wafanyabiashara na wakazi wa maeneo haya na Taifa kwa ujumla, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati.

**(b) Miradi ya Maji**

**(i) Mdari wa majisafi Nzuguni unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umelenga kuongeza upatikanaji wa maji safi katika jiji la Dodoma kutoka uwezo wa awali ambao ulikuwa asilimia 50 ya mahitaji yote. Utekelezaji wa mradi huu ulianza Februari, 2023 utagharimu jumla ya **shilingi bilioni 4.8** na ulikadiriwa kukamilika ndani ya miezi sita. Hata hivyo, utekelezaji haukwenda kama ilivyopangwa hadi Kamati ilipotembelea tena mradi mwezi Januari, 2024 ulikuwa umefikia asilimia 71 ya utekelezaji wake. Kamati ilijulishwa sababu za kutokamilika ni kutopatikana kwa fedha za mradi kwa wakati.

Tathimini iliyofanyika imebainisha kuwa hadi kufikia mwaka 2023 mahitaji ya maji kwa jiji la Dodoma yalikuwa lita 133,400,000 kwa siku na mradi huu ulitegemewa kuongeza upatikanaji wa maji kutoka lita milioni 68 kwa siku hadi kufikia milioni 76.2 kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Serikali kutoa kiasi cha fedha kilichosalia ili mradi huu ukamilike kwa wakati kwa mazingatio kuwa jiji la Dodoma linazidi kukua na mahitaji yanazidi kuongezeka hasa ikizingatiwa kuwa maji ni miongoni mwa mahitaji muhimu sana katika maisha ya mwanadamu ya kila siku.

**(ii) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA)**

**Mheshimiwa Spika**, mamlaka hii inatekeleza ujenzi wa chanzo kipya cha majisafi cha Butimba. Mradi ulikadiriwa kutumia jumla ya **shilingi bilioni 69.34**, na ulianza kutekelezwa tarehe 01 Februari, 2023 kwa makadirio ya kukamilika tarehe 30 Julai, 2021. Kamati ilipofanya ziara katika mradi huu mwezi Machi, 2023 utekelezaji ulikuwa umefikia

asilimia 71. Kamati ilielezwa kwamba, changamoto zinazoukabili mradi huu ni pamoja na utekelezaji wake kuchelewa kuanza kutokana na kuchelewa kupata msamaha wa kodi, jambo lililomkwamisha mkandarasi kuanza kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mradi huu kutaboresha upatikanaji wa majisafi kwa wakazi wa jiji la Mwanza. Kamati inaishauri Serikali kusimamia kiukamilifu mamlaka ili iweze kukamilisha mradi huu na tija ya uwekezaji iweze kupatikana.

**(c) Miradi ya Nishati**

**(i) Mradi wa uzalishaji umeme katika bwawa la Malagalasi**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha maeneo matatu ambayo ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Igamba kwenda Kidahwe yenye urefu wa kilomita 54, ujenzi wa mradi wa bwawa la umeme Malagarasi **(MW 49.5)**, na ujenzi wa njia za usambazaji wa umeme ikiwa ni pamoja na kuunganisha umeme kwenye vijiji saba (7) ambavyo ni Mazungwe, Kidawe, Mwamila, Kalenge, Kazuramimba, Mlela na Igamba.

Gharama za awali za mradi ni **Dola za Marekani milioni 144.14** ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inachangia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 4.14**, na benki ya maendeleo ya afrika (AfDB) inagharamia kiasi cha **Dola za Marekani milioni 140**.

Kukamilika kwa mradi huu kuna manufaa makubwa ikiwemo kuwezesha kuzimwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya Kasulu na Kibondo na TANESCO kuokoa wastani wa **shilingi bilioni 22.38** kwa mwaka zilizokuwa zinatumika kuzalisha umeme katika vituo hivyo, huku mauzo ya umeme yakiwa **shilingi bilioni 6.4** kwa mwaka sawa na asilimia 28 ya gharama za uzalishaji.

Aidha, mradi utawezesha kuwa na umeme wa kutosha katika wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Buhigwe. Umeme unaopatikana sasa kutoka Nyakanazi ni Megawati 12 sawa na ongezeko la takribani asilimia 100 ikilinganishwa na megawati 6.25 zilizokuwa zinazalishwa kwa kutumia mafuta katika vituo vya Kasulu na Kibondo.

**(ii) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kilovoti 400**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha kandarasi tatu ambazo ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400, yenye urefu wa kilomita 280 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma; ujenzi wa vituo viwili vya kupoza umeme msongo wa kilovoti 220/400 cha Nyakanazi na 400/132/33 cha Kigoma vitakavyohusisha ufungwaji wa mashine umba mbili zenye uwezo wa MVA 120 kwa kila moja; na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme msongo wa kilovoti 33 katika vijiji 18 na kuunganisha wateja wa umeme *(last mile connections)* 5,000 katika mkoa wa Kigoma.

Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 186.93** ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inachangia **Dola za Marekani milioni 18.54**, benki ya maendeleo ya Afrika (AfDB) **Dola za Marekani milioni 123.39** na mfuko wa maenedeleo wa watu wa Korea Kusini (EDCF) **Dola za Marekani milioni 45.**

Mradi huu utasaidia kuunganisha umeme wa gridi ya taifa katika mkoa wa Kigoma hivyo kuboresha upatikanaji wa umeme katika mikoa ya magharibi mwa Tanzania; na kuwezesha kuiunganisha Tanzania na nchi jirani za magharibi mwa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukaguzi Kamati ilishauri TANESCO kutekeleza miradi hii kwa wakati ili tuweze kuanza kunufaika na tija ya uwekezaji huu mkubwa uliofanywa na Serikali. Aidha, Kamati

inaisisitiza TANESCO kuhakikisha wakandarasi wanapatiwa mpango wa namna ya kurejesha kwenye jamii (Corporate Social Responsibility - CSR) na kuusimamia ikiwemo kuelimisha wananchi. Hatua hii itasaidia miradi ya TANESCO kugusa jamii inayozunguka mradi husika na kurahisisha utekelezaji wake na hivyo ufanisi na tija kuweza kupatikana.

**(d) Miradi ya utalii na huduma**

**(i) Miradi ya maendeleo katika Hifadhi za Taifa za Kisiwa cha Rubondo na Burigi-Chato**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha miradi miwili ya maendeleo inayolenga kuboresha miundombinu ya malazi ya watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo. Miradi hii ni ujenzi wa malazi ya wageni mashuhuri (VIP Cottage) na ujenzi wa majengo matatu (3) ya malazi ya watalii (2 in 1 Cottages) na inagharimu **shilingi Milioni 544.**

Lengo kuu la miradi hii ni kuongeza uwezo wa malazi ya kitalii na mapato ya Serikali kupitia huduma ya malazi kwa wageni wa ndani na nje wanaotembelea hifadhi. Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza uwezo wa hifadhi ya Rubondo kuwahudumia watalii na kuongeza pato litokanalo na utalii kwa ujumla. Ni ushauri wa Kamati kwamba, mamlaka husika isimamie kikamilifu kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati.

**(ii) Ujenzi wa Hotel ya Nyota Tano Jijini Mwanza**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusu ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tano mkoani Mwanza (Mwanza Tourism) unaotekelezwa na mfuko wa taifa wa hifadhi ya jamii (NSSF). Utekelezaji wake ulianza mwaka 2010 kwa matarajio ya kukamilika Oktoba, 2016 kwa gharama ya **shilingi bilioni 89.9.** Hata hivyo, mradi huu haukukamilika kwa wakati

kutokana na changamoto ya kutokupatikana kwa mwendesha hoteli (hotel operator), hali iliyosababisha mchakato huo kurudiwa mara mbili katika nyakati tofauti (mwaka 2017 na 2018) na baada ya kushindikana katika vipindi hivyo, mchakato ulilazimika kusubiri ili kupisha changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 na ulirejea mwaka 2022.

Mfuko ulirudia mchakato kwa kutangaza tena zabuni hiyo kimataifa ambapo kampuni za Hilton Hotels Worldwide, Radissons Hotels na Legacy Hotel zilijitokeza kuomba kazi, na mchakato wote unatarajia kukamilika Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu utasaidia kukuza utalii na kuunganisha shughuli za uvuvi na madini ambazo kiujumla ndizo zinaleta wageni kutoka mataifa mbalimbali. Kutokana na faida za mradi huu katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii, pamoja na kuhakikisha uendelevu na urejeshwaji wa fedha za wanachama, kamati inaishauri NSSF ihakikishe inakamilisha mradi huu katika muda uliotajwa ili manufaa na tija ya mradi ianze kupatikana.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwezi Machi, 2023, Kamati ilitoa ushauri wa jumla ufuatao kwa Serikali:-

(i) Kuhakikisha mikataba ya utekelezaji wa miradi hasa inayotekelezwa na wakandarasi wa nje, inaweka kipengele cha kushirikisha wataalamu wa ndani na kuandaa mpango wa kurithisha maarifa *(knowledge transfer and succession plan*) ili kuwawezesha kusimamia na kuendesha miradi baada ya makabidhiano;

(ii) Kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati ili kuhakikisha inakamilika na tija ya uwekezaji inaanza kupatikana;

(iii) Kuhakikisha taasisi na mashirika ya umma yanaandaa mpango wa uwekezaji na kuutekeleza kikamilifu kwa lengo la kuyawezesha kupanga utekelezaji wa miradi kulingana na rasilimali zilizopo kwa wakati;

(iv) Kusimamia kikamilifu wakandarasi ili kuhakikisha wanatekeleza miradi kulingana na matakwa ya mikataba waliyoingia ili kuepuka tabia ya kuongeza muda bila sababu za msingi, na hivyo kukamilisha miradi kwa wakati na kupata tija ya uwekezaji;

(v) Kuhakikisha wakandarasi wanakuwa na mpango wa kurejesha kwa jamii (Corporate Social Responsibility - CSR). Jambo hili linaziwezesha jamii husika kuona zimehusishwa hivyo kuleta ushirikiano katika utekelezaji wa miradi husika; na

(vi) Kuweka miundombinu ya reli na barabara kwa kiwango cha lami kwa upande wa bandari za ukanda wa magharibi (Karema na Mpanda) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa bandari hizi.

## 2.5 Ushiriki katika Semina na warsha Mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina na warsha mbalimbali ambazo zililenga kuwajengea uwezo. Kamati inawashukuru wadau wote ambao walijitokeza katika kutoa semina za mafunzo na kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati. Semina na warsha hizo zimekuwa na manufaa katika kuongeza uelewa wa Wajumbe wa mambo mbalimbali yanayohusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma hivyo kuiwezesha Kamati kutoa ushauri wenye tija. Ni imani ya kamati kuwa ushirikiano huo utaendelea katika kuijengea kamati uwezo kwa maslahi mapana ya taifa letu.

## SEHEMU TATU

## 3.0 MAONI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati hii ni tegemeo la Bunge katika kufuatilia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Maoni yake yanahusu namna Serikali inavyoweza kutumia Mitaji ya Umma. Kutokana na uchambuzi na ufuatiliaji uliofanywa na Kamati, yapo mambo maalumu yanayotolewa maoni na mapendekezo kwa madhumuni ya kulisaidia Bunge kujadili na kuamua. Kwa ujumla mambo makuu yanayojitokeza katika Taarifa hii ni pamoja na:-

3.1.1 STAMIGOLD na ETDCO kuchelewa kupewa marejesho ya VAT, jumla ya sh. Bilioni 15.9 ambazo ni marejesho ya VAT kwa STAMIGOLD, GASCO na ETDCO ni kiasi ambacho kinaathiri ufanisi katika uwekezaji kutokana na kupungua kwa mtaji.

3.1.2 Baadhi ya taasisi na Mashirika ya Umma kushindwa kuzingatia vigezo vya utendaji, licha ya Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370 kumpa Msajili wa Hazina uwezo wa kupanga vigezo vya utendaji;

3.1.3 Taasisi za uwekezaji kujiendesha bila kuwa na mpango wa uwekezaji, jambo linaloathiri Mitaji ya Umma iliyowekezwa kwa taasisi hizo;

3.1.4 Uanzishwaji wa Kampuni Tanzu za Taasisi za uwekezaji wa mitaji ya Umma, ambapo imabainika badhi ya kampuni tanzu zinazozorotesha ufanisi wa mitaji ya umma ni jambo linalokinzana na madhumuni ya kuanzishwa kwake;

3.1.5 Kushindwa kwa Benki ya Maendeleo kujiendesha ambapo imebainika kuwa Benki hii inakabiliwa na changamoto ya kuwa

na mtaji mdogo, kushindwa kukidhi masharti ya Benki ya Tanzania kuhusu kiwango cha mtaji na kushindwa kulipa amana zilizowekwa na watu na taasisi za Serikali;

3.1.6 Bodi ya Utalii Tanzania inakabiliwa na changamoto ya sheria iliyoianzisha kuwa imepitwa na wakati na Bodi inauwezo mdogo wa kifedha unaochangiwa na kuondolewa kwa ushuru wa utalii na taasisi nyingine kuendelea kujitangaza;

3.1.7 Baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuathiriwa na Madeni;

3.1.8 Changamoto ya Upatikanaji wa Rejesho la Uwekezaji;

3.1.9 Utendaji wa Mamlaka za Maji ambapo Mamlaka za Maji zinajumuishwa kwenye malipo ya gharama za umeme kibiashara jambo linalosababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

## 3.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza Shughuli za Kamati na maoni ya jumla, naomba kutoa Mapendekezo kama ifuatavyo:-

### 3.2.1 Taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma kucheleweshewa marejesho ya VAT

**KWA KUWA,** Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) inayopaswa kurudishwa kwa wahusika inachelewa kuzifikia taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma kama vile STAMIGOLD, ETDCO na GASCO,

**NA KWA KUWA,** kuchelewa kurejeshwa kwa VAT kunaathiri ukwasi kwa taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma zikiwemo zilizotajwa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma zinarejeshewa VAT haraka mara baada ya kukamilika kwa taratibu stahiki.

### 3.2.2 Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kushindwa kuzingatia vigezo vya utendaji

**KWA KUWA,** imebainika kuwepo kwa baadhi ya taasisi na mashirika yanayotumia Mtaji wa Umma ambayo yanajiendesha bila kuzingatia vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina.

**NA KWA KUWA,** athari ya taasisi na mashirika hayo kutokuzingatia vigezo inabainika kwenye ufanisi na tija ya uwekezaji wa Mitaji ya Umma inayotumika,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

(i) Serikali iongeze usimamizi wa Bodi na Menejimenti za Mashirika na taasisi zinazotumia Mtaji wa Umma katika uwekezaji; na

(ii) Sambamba na kuongeza usimamizi, Serikali ikamilishe mchakato wa uandaaji wa Muswada wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma ya Mwaka 2023 na kuurejesha Bungeni ili Sheria hii iweze kutungwa wa lengo la kuongeza nguvu katika usimamizi wa mashirika ya umma na tija ya uwekezaji wa mitaji kuweza kupatikana.

### 3.2.3 Baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Umma kufanya Shughuli za Uwekezaji bila kuwa na Mpango wa Uwekezaji (Investment Plan)

**KWA KUWA**, zipo baadhi ya taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma zinazojiendesha bila kuwa na Mpango wa uwekezaji,

**NA KWA KUWA,** taasisi zinazojiendesha bila Mpango wa Uwekezaji zinakosa mwongozo na mikakati inayolenga tija na hivyo kutokuwa na ufanisi katika uwekezaji,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze usimamizi wa taasisi za uwekezaji ili ziweze kuandaa mpango wa uwekezaji na kuutekeleza kiukemilifu kwa lengo la kuongeza ufanisi.

### 3.2.4 Uanzishwaji wa Kampuni tanzu za Taasisi za Uwekezaji wa Umma usiosimamiwa vema

**KWA KUWA,** uanzishwaji wa Kampuni tanzu unaolenga kuzisaidia Kampuni mama kujiendesha kibiashara umebainika kushindwa kufanikisha azma hiyo kutokana na kukosekana kwa usimamizi wa utaratibu wake,

**NA KWA KUWA,** kushindwa kwa baadhi ya Kampuni tanzu za taasisi za Uwekezaji wa Umma:-

(i) Kunatokana na kukosekana kwa usimamizi Madhubuti wa taratibu za uendeshaji wake;

(ii) Kunaathiri ufanisi wa Kampuni mama iliyotarajiwa kunufaika na Kampuni tanzu; na

(iii) Ni suala linalo hukwamisha ufanisi wa Mtaji wa Umma unaotumika katika taasisi ya uwekezaji wa umma.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) Ifanye tathmini ya kina kubaini iwapo Kampuni tanzu zilizoanzishwa na taasisi za uwekezaji wa mitaji ya umma zina umuhimu, tija na manufaa katika uwekezaji;

(ii) Iweke mfumo mzuri wa usimamizi wa uanzishaji wa Kampuni tanzu unaozingatia umuhimu wa uanzishaji wa kampuni tanzu na kufanya maandalizi yote kwa mujibu wa Muongozo uliowekwa na Msajili wa Hazina; na

(iii) Ianze mchakato wa marekebisho ya sheria inayoweka masharti ya lazima kwa Msajili wa Hazina kupewa angalau hisa chache katika Kampuni tanzu ili aweze kuwa na uangalizi wa karibu.

### 3.2.5 Kushindwa kwa Benki ya Maendeleo kujiendesha

**KWA KUWA,** Benki ya Maendeleo (TIB) iliyoanzishwa kwa lengo la kutoa huduma za kifedha kwenye miradi ya maendeleo, inakabiliwa na ukata wa mtaji na kwamba:

(i) Ina mtaji mdogo wa kiasi cha shilingi bilioni 24;

(ii) Haikidhi masharti ya Benki Kuu ya Tanzania ya kuwa na mtaji usiopungua shilingi Bilioni 200;

(iii) Imeshindwa kulipa amana za jumla ya shilingi bilioni 206.854 zilizowekwa na watu binafsi na baadhi ya taasisi za Serikali

(iv) Imepata hasara ya kiasi cha shilingi bilioni 195.91 kati ya mwaka 2021 na 2022 kutokana na tengo la mkopo chechefu hadi asilimia 20 ili hali ukomo wa BOT ni tengo la asilimia 5.

**NA KWA KUWA**, Hali hiyo inatofautiana kabisa na lengo la kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo na kwamba, inakwamisha uwekezaji wa watu na taasisi za Serikali,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali -

(i) Ifanyike tathmini ya kubaini umuhimu, uendeshaji na ustahimilivu wa Benki ya Maendeleo ili kuchukua hatua stahiki;

(ii) Isimamie Benki ya Maendeleo na kuhakikisha kuwa Benki hiyo inajielekeza katika kutekeleza majukumu yake ya msingi bila kuendelea na shughuli zilizo nje ya malengo ya kuanzishwa kwake;

(iii) Isimamie kwa dhati na kufuatilia kwa karibu wadaiwa sugu ili waweze kulipa madeni yao kwa lengo la kuongeza ukwasi wa Benki hii; na

(iv) Ihakikishe kuwa amana zinazodaiwa na watu binafsi na taasisi za Serikali yanalipwa ili kupunguza madhara kwa wadai au taasisi hizo.

### 3.2.6 Changamoto ya Bodi ya Utalii Tanzania kutokana na Sheria iliyoianzisha

**KWA KUWA,** Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364 ina ufanisi mdogo kutokana na -

(i) Kuondolewa kwa ushuru wa utalii tangu mwaka 2020/21 uliokuwa unatumika kwa uendeshaji wa Bodi; na

(ii) Kuwepo kwa taasisi nyingine za utalii zinazotangaza masuala ya utalii kama inavyotekelezwa na Bodi ya utalii.

**NA KWA KUWA**, Hali hiyo inakwamisha uwezo wa kibajeti wa Bodi ya Utalii, jambo ambalo linaathiri utendaji wake na ufanisi wa mtaji.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Ianze mchakato wa kuhuisha Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania iliyotungwa mwaka 1962 ili kuwezesha Bodi hii kuendana na wakati;

(ii) Ihakikishe kuwa marekebisho ya Sheria yanaendana na kuibadili Bodi ya Utalii Tanzania, iwe Mamlaka ya Utalii Tanzania (*Tanzania Tousim Authority – TTA*); na

(iii) Ifanye jitihada za kurejesha ushuru wa utalii kwenye shughuli za Bodi ya Utalii Tanzania.

### 3.2.7 Baadhi ya Taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuathiriwa na madeni zinazodai taasisi za Serikali.

**KWA KUWA,** imebainika kuwa taasisi za uwekezaji wa mitaji ya umma zinazodai taasisi nyingine za Serikali zinaathirika katika mitaji yake kama vile:-

(i) ETDCO inayoidai TANESCO na REA inaathrika katika mtaji wake kwa kiasi cha shiling Bilion 44.782; na

(ii) LATRA inayoidai TRC na UDART inaathirika katika mtaji wake kwa kiasi cha shilingi Bilioni 3.7.

**NA KWA KUWA**, athari hiyo ya mtaji inayotokana na madeni ambayo taasisi za uwekezaji zinadai (Receivables) inakwamisha tija na ufanisi wa uwekezaji,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) Ihakikishe kuwa taasisi zote za Serikali zinazodaiwa na taasisi za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, zinalipa madeni haraka inavyostahili; na

(ii) Iweke mfumo Madhubuti wa kusimamia na kuziwajibisha taasisi zinazopokea huduma kutoka taasisi za uwekezaji wa mitaji ya umma ili zilipe huduma hizo kwa wakati.

### 3.2.8 Changamoto ya upatikanaji wa Rejesho la Uwekezaji (Returns on Investment)

**KWA KUWA**, Uwekezaji wa umma unatarajiwa kuipatia Serikali rejesho kwa njia ya gawio na michango mingine lakini -

(i) Baadhi ya taasisi haziwasilishi kabisa gawio au michango;

(ii) Baadhi ya taasisi zinazowasilisha gawio au michango zinawasilisha kwa kiasi kidogo kuliko inavyotakiwa; na

(iii) Baadhi ya taasisi zinazowasilisha gawio au michango mingine zinawasilisha kwa kuchelewa.

**NA KWA KUWA,** changamoto hiyo ya taasisi kutoa gawio au michango kwa Serikali kwa tabu inatokana na :-

(i) Usimamizi usio Madhubuti wa Serikali; na

(ii) Kutokuwajibika ipasavyo kwa bodi na menejimenti za taasisi zinazohusika.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) Iongeze na kuimarisha usimamizi wa uendeshaji wa taasisi na mashirika ya umma yanayotumia mtaji wa umma ili zitoe gawio na michango kwa mujibu wa Sheria; na

(ii) Iwajibishe bodi na menejimenti za taasisi ambazo hazitekelezi sharti la kisheria kuhusu gawio na michango.

### 3.2.9 Mamlaka za Maji kutozwa gharama za Huduma ya Umeme kibiashara

**KWA KUWA,** Mamlaka za maji ambazo ni taasisi za huduma hulipia gharama za umeme kwa mpango wa matumizi ya kibiashara badala ya huduma,

**NA KWA KUWA,** Mpango huo wa ulipaji unaziongezea mamlaka za maji gharama za uendeshaji na kuzipunguzia ufanisi wa mtaji,

**NA KWA KUWA,** tozo (tariff) za maji hazijabadilika kwa muda mrefu sasa toka mwaka 2015 licha ya gharama nyingine za uendeshaji kubadilika na kuathiri uwiano wa mapato na matumizi ya mamlaka za maji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali

(i) Ifanye tathmini ya gharama za uendeshaji wa mamlaka za maji kwa lengo la kuzipunguzia;

(ii) Iwezeshe mamlaka za maji kulipia bei za kihuduma kwa lengo la kuzipunguzia gharama za uendeshaji; na

(iii) Ifanye mapitio ya tozo (tariff) za maji ili ziweze kuendana na gharama za uzalishaji na.

### 3.2.10 Mamlaka za Maji kuongezewa mzigo wa kugharamia miradi ya maji taka

**KWA KUWA,** imebainika kwamba mamlaka za maji zinategemea mapato kutoka kwenye huduma ya maji safi kuliko maji taka, lakini uwekezaji katika miundombinu ya maji taka ni juu zaidi ya ile ya maji safi,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo inaziweka Mamlaka za Maji kuwa na matumizi makubwa kuliko mapato, jambo linalopunguza mtaji wa mamlaka hizo.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali izipatie Mamlaka za Maji fedha za kugharamia miradi ya mazingira kama ilivyo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na NEMC ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa jukumu la usimamizi wa mazingira.

### 3.2.11 Changamoto ya uendeshaji wa NARCO

**KWA KUWA,** NARCO inakabiliwa na changamoto za kiuendeshaji ikiwemo tozo ndogo kwa watumiaji wa vitalu vyake, kutojulikana kwa idadi na ukubwa halisi wa Ranchi zinazo milikiwa na NARCO na ufinyu wa fedha;

**NA KWA KUWA,** changamoto hizo zinachangia ufanisi na tija ndogo ya NARCO,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali -

(i) Ifanye tathmini ya utendaji wa NARCO na kuiwezesha kuandaa mpango kabambe wa mabadiliko (turn around strategy) wa kampuni na kuutekeleza ili kuibadili kampuni kiutendaji, kuongeza ufanisi na kuleta tija ya uwekezaji;

(ii) Ifanye uhakiki wa ukubwa wa vitalu vya NARCO na wapangishwaji kwa lengo la kubaini kama kuna udanganyifu unaofanyika katika mikataba ya ukodishwaji iliyotolewa;

(iii) Ifanye tathimini juu ya gharama za ukodishaji wa vitalu kwa kushabihisha faida ipatikanayo kwa wanaoendesha

vitalu hivi kwa lengo la kujua gharama halisi inayopaswa kutozwa; na

(iv) Iwekeze kiasi kilichopangwa katika mpango mkakati wa kampuni ya NARCO wa miaka 10 ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini katika kuliongoza Bunge letu tukufu ikiwa ni pamoja na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri, miongozo na msaada uliotupatia kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Pia, naomba nimshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuendesha Bunge.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora wa taasisi na mashirika ya umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa taifa ikiwa ni pamoja kufanya uamuzi wa kuanzisha Wizara mahususi ya usimamizi wa uwekezaji ambayo ni Wizara ya Mipango na Uwekezaji chini ya Ofisi yake na kisha kuiweka Ofisi ya Msajili wa Hazina chini ya usimamizi wa Wizara ya Mipango ya uwekezaji kwa nia ya kuisimamia kwa ukaribu. Pia, ameridhia kutungwa kwa Sheria ya Uwekezaji wa Umma ya Mwaka 2023, kutungwa kwa sheria hiyo kutaleta mageuzi katika uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma kwa kuweka mfumo madhubuti wa kisheria na kitaasisi wa kusimamia mashirika na taasisi za umma. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali ikamilishe mchakato wa Muswada huu ili sheria hii iweze kutungwa na kuanza kutumia

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha

mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Naomba kuwatambua wajumbe kwa majina yao kama yanavyoonekena hapo chini:-

1. Mhe. Deus Clement Sangu, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Augustine Vumma Hole,Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb
4. Mhe. Aeshi Alfan Hillary, Mb
5. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
6. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb
7. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb
8. Mhe. Bonah Ladislaus Kamoli, Mb
9. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
10. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb
11. Mhe. Mary Fransis Msanja , Mb
12. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb
13. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb
14. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb
15. Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
16. Mhe. Fratey Gregory Massay Mb
17. Mhe. George Natany Malima, Mb
18. Mhe. Haji Amour Haji , Mb
19. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb
20. Mhe. Matha Nehemia Gwau, Mb
21. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb
22. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina wakiongozwa na Msajili wa Hazina Ndg.Nehemia Mchechu kwa ushirikiano wa dhati walioutoa kwa Kamati. Wamesaidia kushauri namna bora ya kuzisaidia taasisi na

mashirika ya umma, kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija ya uwekezaji wa Serikali katika vitega uchumi vyake.

**Mheshimiwa Spika**, pia napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc)*, kwa ushirikiano walioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati.

## 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imetokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*PIC*) kuhusu utekelezaji na usimamizi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi huu, yanalenga kuishauri serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji uweze kufanyika kwa ufanisi na hatimaye kuleta tija kwa taifa.

Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa liipokee taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kipindi Mwaka 2023, kuijadili na hatimaye kuridhia maoni na mapendekezo yake ili Serikali iweze kuyafanyia kazi**.**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

Deus Clement Sangu, Mb.

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

13 Februari, 2024

## VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1**

TAASISI NA MASHIRIKA YALIYOKUTANA NA KAMATI YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI, 2023 HADI JANUARI, 2024

| NA. | JINA LA TAASISI/SHIRIKA |
|---|---|
| 1. | Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) |
| 2. | Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) |
| 3. | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) |
| 4. | Shirika la Mawasiliano Tanznaia (TTCL) |
| 5. | Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC) |
| 6. | Kampuni ya Mbolea (TFC) |
| 7. | Shirika la Bima la Taifa (NIC) |
| 8. | Mfuko wa Taifa wa Maji (NWF) |
| 9. | Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) |
| 10. | Bodi ya Mikopo (HESLB) |
| 11. | Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) |
| 12. | Malaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) |
| 13. | Mamlaka ya Usimamizi wa Anga Tanzania (TCAA) |
| 14. | Mzinga Cooperation |
| 15. | Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) |
| 16. | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) |
| 17. | Shirika la maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) |
| 18. | Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) |
| 19. | Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) |
| 20. | Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) |
| 21. | Wakala wa Nishati Vijijini (REA) |
| 22. | TANESCO katika Grid Imara na katika Bwawa la Nyerere |

| NA. | JINA LA TAASISI/SHIRIKA |
|---|---|
| 23. | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) |
| 25. | Chuo kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) |
| 26. | Chuo kikuu cha Ardhi (ARU) |
| 27. | Kampuni ya Uendeshaji Kiwanda cha Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro KADCO |
| 28. | Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) |
| 29. | Mamlaka ya Mafunzo ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) |
| 30. | Sokoine University of Agriculture (SUA) |
| 31. | Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) |
| 32. | Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF) |
| 33. | Shirika la Posta Tanzania (TPC) |
| 34. | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) |
| 35. | Tume ya Nishati ya Atomiki Tanzania (TAEC) |
| 36. | Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) |
| 37. | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) |
| 38. | Bohari ya Dawa (MSD) |
| 39. | Bodi ya Chai Tanzania (TBT) |
| 40. | Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) |
| 41. | Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) |
| 42. | Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) |
| 43. | Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) |
| 44. | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) |
| 45. | Mamlaka ya Maji ya Tanga (TANGAUWASA) |
| 46. | Mamlaka ya Maji Safi na Usimamizi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) |
| 47. | Mfuko wa Self (SELF) |
| 48. | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) |
| 49. | Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) katika Kampuni Tanzu za |

| NA. | JINA LA TAASISI/SHIRIKA |
|---|---|
| | i. STAMIGOLD Company Limited; na<br>ii. Buhemba Gold Company Limited. |
| 50. | Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) kwenye kampuni Tanzu za<br>i. Electrical Transmission And Distributions Constructions And Maintenance Company Limited (ETDCO ); na<br>ii. Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company LTD (TCPM). |
| 51. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (*PSSSF*) kwenye Kampuni Tanzu ya<br>i. Azania Bank; na<br>ii. International House Property. |
| 52. | Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) katika Kampuni Tanzu ya -<br>i. Tanzania Oil Investment (TANOIL); na<br>ii. GAS Company (GASCO). |
| 53. | Benki ya Maendeleo Tanzania (TIB Development) |
| 54. | Benki ya Maendeleo ya kilimo Tanzania (TADB) |
| 55. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) |
| 56. | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) |
| 57. | Shirika la Viwango Tanzania (TBS) |

**Kiambatisho Na. 2**

**JEDWALI KUONYESHA MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOKAGULIWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KATIKA ZIARA YA KAMATI (14 MACHI, 2023 HADI 01 APRIL, 2023)**

| TAREHE | MKOA | MRADI | TAASISI | THAMANI YA MRADI (TSH) | HATUA YA UTEKELEZAJI WA MRADI | MUDA WA MRADI KUANZA | MUDA WA MRADI KUKAMILIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 Machi, 2023 | DODOMA | Majisafi Nzuguni | DUWASA | Bilioni 4.8 | 5% | 07 Februari, 2023 | 07 Agosti, 2023 |
| | | Mradi wa Iyumbu (Nyumba 300) | NHC | Bilioni 16.6 | 95% | 06 Januari, 2021 | 30 Aprili, 2023 |
| | | Mradi wa Chamwino | | Bilioni 7.9 | 90% | 06 Januari, 2021 | 30 Aprili, 2023 |
| 16 Machi, 2023 | TABORA | Majisafi Kutoka Ziwa Viktoria hadi Mkoa wa Tabora | TUWASA | Bilioni 617.3 | 100% | Mwaka 2004 | Februari, 2020 |
| 17 Machi, | | Ukarabati wa Chuo cha Reli na Karakana ya Reli | TRC | Milioni 914.3 | 100% | Mwaka 2020 | Mwaka 2022 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2023 | | Tabota | | | | | |
| | KATAVI | Ujenzi wa Bandari ya Karema | TPA | Bilioni 47.97 | 99% | 25 Oktoba, 2021 | 20 Mei, 2022 |
| 20 Machi, 2023 | | Kuzalisha Umeme kwa Mitambo ya Mafuta kwenye Majenereta ya Bangwe | TANESCO | Bilioni 50 | 100% | | Mradi umekamilika na unafanya kazi. |
| 21 Machi, 2023 | | Ukarabati wa Meli ya Mt Sangara | MSCL | Bilioni 8.34 | 90.7% | 08 Novemba, 2021 | 31 Machi, 2023 (Mkandarasi amepatiwa nyongeza ya mwezi mmoja) |
| 22 Machi, 2023 | KIGOMA | **Lot 1** - Kasulu hadi Manyovu (68.25km) pamoja na barabara ya kuingia Kasulu Mjini. | TANROADS | Bilioni 80.1 | 45.52% | 14 Septemba, 2020 | 13 Septemba, 2023 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Lot 2** - Makutano ya Kanyani hadi Mvugwe (70.5kms). | | Bilioni 87.8 | 52.89% | 23 Oktoba, 2020 | 23 Oktoba, 2023 |
| | | **Lot 3** - Mvugwe hadi Makutano ya Nduta (59.35kms). | | Bilioni 88.0 | 61.83% | 10 Oktoba, 2020 | 26 Oktoba, 2023 |
| | | **Lot 4** -Makutano ya Nduta hadi Kabingo (62.5kms) | | Bilioni 85.1 | 75.6% | 17 Desemba, 2020 | 17 Desemba, 2023 |
| 23 Machi, 2023 | KAGERA (BIHARAMULO-NYAKANAZI) | Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa Kilovolti 400 Nyakanazi hadi Kigoma | TANESCO | Bilioni 429.93 | 41% | Januari, 2022 | Januari, 2024. |
| 24 Machi, 2023 | GEITA (CHATO) | Ujenzi wa malazi ya wageni Mshuhuri eneo la Kageye | TANAPA | Milioni 257.7 | 65% | 03 Novemba, 2021 | 03 Aprili, 2023 |
| | | Ujenzi wa Malazi sita ya Watalii (2 | | Milioni | 98% | 22 Septemb | 26 Machi, |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa 1) | | 753.6 | | a, 2021 | 2023 |
| | | Ujenzi wa Kituo cha Kutolea Taarifa za Hifadhi kwa Watalii Hifadhi ya Burigi Chato | | Milioni 392.9 | 98% | 02 Machi, 2022 | 16 Aprili, 2023 |
| | | Ujenzi wa majengo matatu ya malazi ya watalii eneo la Kageye | | Milioni 430.8 | 65% | 31 Mei, 2022 | 15 Aprili, 2023 |
| 25 Machi, 2023 | MWANZA | Ujenzi wa Daraja la J.P Magufuli (Kigongo Busisi) | TANROADS | Bilioni 716.333 | 70% | 25 Februari, 2020 | 24 Februari, 2024 |
| 26 Machi, 2023 | | Ujenzi wa Kiwanda Cha Kusafisha Dhahabu cha Mwanza Precious Metals | STAMICO | 16.5 bilioni | 100% | 15 Machi, 2020 | Desemba, 2020 |
| 27 Machi, 2023 | | Ujenzi wa Meli ya Mv Mwanza Hapa Kazi tu na | MSCL | 108.5 bilioni | 82% | Januari, 2019 | Agosti, 2023 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ukarabati wa Meli ya Mv Umoja | MSCL | 19.8 bilioni | 71% | 25 Novemba, 2021 | 28/02/2023 (Ombi la muda wa nyongeza linafanyiwa kazi na MSCL) |
| 28 Machi, 2023 | | Ujenzi wa Reli ya SGR Kipande cha Tano Kutoka Mwanza hadi Isaka | TRC | Trilioni 3.06 | 28.03% | Mei, 2021 | Mei, 2024 |
| 29 Machi, 2023 | | Ujenzi wa Kiwanda cha Kukoboa Mpunga Butimba | CPB | Bilioni 3.68 | 100% | Agosti, 2020 | Desemba, 2021 |
| | | Ujenzi wa Chanzo Kipya cha Majisafi Butimba | MWAUWASA | Bilioni 69.34 | 71% | 01 Februari, 2021 | 30 Julai, 2023 |
| 30 Machi, 2023 | | Kitegauchumi cha Jengo la Kibiashara (The Rock City Mall) | PSSSF | Bilioni 80.35 | 100% | Agosti, 2012 | Machi, 2015 |
| | | Ujenzi wa Hoteli ya Hadhi ya | NSSF | Bilioni | 74% | Novemb | Juni, 2024 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Nyota Tano ya Mwanza Tourist | | 89.90 | | a, 2013 | |
| 1 April, 2023 | SINGIDA | REA III ROUND II-Mkoa wa Singida | REA | Bilioni 58.014 | 62.87% | 4 Novemba, 2021 | Desemba, 2023 |
| **JUMLA** | | | | **Trilioni 8.5** | | | |